TANGAZO LA SERIKALI Na. 223 la tarehe 15/4/2022

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*Iimetungwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1)*

## SHERIA NDOGO YA USHURU WA MAZAO YA MISITU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO YA MWAKA 2022

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Misitu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo ya Mwaka, 2022.

Eneo la kutumika

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo: -

“Afisa Mwidhiniwa” maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo;

“mazao ya misitu” maana yake ni mbao, nguzo ndogo (Milunda), nguzo kubwa, mkaa, fito na magogo mabichi na makavu;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri na ni pamoja na Afisa yeyote atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnunuzi" maana yake ni mtu, kikundi cha watu au taasisi inayotambuliwa chini ya sheria za nchia mbayo inajihusisha na biashara ya mazao ya misitu ndani na nje ya Halmashauri;

"muuzaji" maana yake ni mtu, kikundi cha watu au taasisi inayotambuliwa chini ya sheria za nchi inayojishughulisha na uzalishaji au uuzaji wa mazao ya misitu ndani ya Halmashauri' isipokuwa muuzaji ambaye ni mkulima;

"ushuru" maana yake ni ushuru wa mazao ya misitu utakaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii;

"wakala" maana yake ni mtu, kikundi cha watu au taasisi inayotambuliwa chini ya sheria za nchi atakayeteuliwa na Halmashauri kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Leseni ya biashara ya mazao ya misitu

4. (1) Kila muuzaji wa mazao ya misitu ndani ya eneo la Halmashauri atatakiwa kuwa na leseni ya kuendesha biashara ya mazao ya misitu.

(3) Mtu yeyote atakayefanya biashara ya kuuza mazao ya misitu bila ya kuwa na leseni iliyotolewa na Halmashauri atakuwa ametenda kosa.

Ushuru wa mazao ya misitu

5. (1) Kila mnunuzi wa mazao ya misitu ndani ya Halmashauri atatakiwa kulipa ushuru kwa kiwango cha asilimia tano ya bei ya kununulia.

(2) Mnunuzi atatakiwa kulipa ushuru kwa Afisa Mwidhiniwa au Wakala na atawajibika kudai risiti ya kielektroniki.

Uteuzi wa Wakala

6 (1) Halmashauri inaweza kumteua Wakala kwa madhumuni ya kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala atakayeteuliwa na Halmashauri atakuwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Uanzishwaji wa Vituo vya ukaguzi wa mazao ya misitu

7\. (1) Halmashauri inaweza kuanzisha vituo mbalimbali ndani ya Halmashauri kwa madhumuni ya kukagua mazao ya misitu yanayosafirishwa kutoka ndani ya mamlaka ya Halmashauri.

(2) Ukaguzi wa mazao ya misitu Vituoni utahusisha uhakiki wa nyaraka za uuzaji na ununuzi wa zao husika na ushuru uliolipwa.

Usafirishaji wa mazao ya misitu

8\. (1) Kila msafirishaji wa mazao ya misitu ndani ya eneo la Halmashauri atatakiwa kujaza fomu maalumu zilizoambatishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii na atahakikisha kuwa ana: -

(a) kibali cha kuvuna mazao ya misitu;
(b) kibali cha kununua mazao ya misitu;
(c) nakala ya stakabadhi ya ushuru uliolipwa na muuzaji au mnunuzi wa mazao hayo; na
(d) leseni ya biashara ya mazao ya misitu.

Kutaifisha

9\. Halmashauri inaweza kutaifisha na kuuza mazao ya misitu yaliyouzwa au kununuliwa bila kufuata masharti ya Sheria Ndogo hii, baada ya kuomba na kupata kibali cha Mahakama kwa madhumuni hayo.

Adhabu

10\. Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na endapo atatiwa hatiania atahukumiwa adhabu ya kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi

ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

11. Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mtu huyo atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe kwa kujaza Fomu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili na kukubali kutekeleza wajibu wake.

JEDWALI LA KWANZA
(limetungwa chini ya kifungu cha 8

FOMU NAMBA 1

KIBALI CHA KUVUNA MAZAO YA MISITU

*(Chini ya kifungu cha 8)*

1. Jina la Muuzaji/Mvunaji:_____________________________________________
2. Anuani S.L.P___________mji/kijiji_____________kitongoji______________ Simu____________________
3. Mahali anapoishi Mji/Kijiji ________________ Kitongoji:________________
4. Aina ya zao analotaka kukata:_________________________________________
5. Jina la Mnunuzi:__________________________Anuani__________________
6. Kiasi cha Mazao kichovunwa/uzwa:___________________________________
7. Namba ya leseni ya biashara ya mazao ya misitu_______________________

MIMI________________________________________NAAPA / NATHIBITISHA kwamba nitauza mazao yangu ya misitu Kwa kuzingatia matakwa ya Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Mazao ya Misitu) ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo za Mwaka, 2022 kwa kuzingatia kipimo cha mita za ujazo katika kutoza bei na sio Vinginevyo. Pia natambua kuwa kuuza mazao hayo kinyume na matakwa ya Sheria Ndogo hizi ni kosa na nastahili adhabu.

Saini ya Mwombaji:____________________________________________________Alama ya dole gumba__________________________________

Tarehe ya kusaini kibali:_______________________________________________

Jina la Afisa Mtendaji wa Kijiji:________________________________________

Saini ya Afisa Mtendaji:_______________________________________________

Mhuri wa Mtendaji wa Kijiji:___________________________________________

FOMU NAMBA 2

KIBALI CHA KUNUNUA MAZAO YA MISITU

1. Jina la Mnunuzi:_________________________________________________
2. AnuaniS.L.P___________Mji/kijji______________kitongoji______________
3. Simu ____________________
4. Aina ya zao analotaka kununua:_____________________________________
5. Jina la Muuzaji:____________________anuwani _________________
6. Kiasi cha Mazao kitachonunuliwa:____________________________________

MIMI_____________________________________________NAAPA / NATHIBITISHA; kwamba nitanunua mazao ya misitu kwa kuzingatia matakwa ya Sheria Ndogo ya ( Ushuru wa Mazao ya Misitu) ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo, 2022 kwa kuzingatia kipimo cha mita za ujazo katika kulipa bei na sio Vinginevyo. Pia natambua kuwa kununua mazao hayo kinyume na matakwa ya Sheria Ndogo hizi ni kosa na nastahili adhabu.

Saini ya Mwombaji:____________________________________________________

Alama ya dole gumba la Mwombaji________________________________________

Tarehe ya kusaini kibali:_________________________________________________

Jina la Afisa Mtendaji wa Kijiji:__________________________________________

Saini ya Afisa Mtendaji:_________________________________________________

Mhuri wa Mtendaji wa Kijiji:_____________________________________________

___________

JEDWALI LA PILI

____________

(Limetungwa chini ya kifungu cha 11)

HATI YA KUFIFILISHA KOSA

Mimi:_________________________________________nakiri mbele ya Bw/Bi:______________Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri yaWilaya ya Kilolo kwamba tarehe:_______________ya mwezi_________mwaka___________nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu chaa__________________cha Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Misitu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo ya Mwaka 2022.

Nipo tayari kulipa kiasi Shilingi laki mbili badala ya kushtakiwa Mahakamani.

Nathibitisha kwamba maelezo ya hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu kadri ya ufahamu wangu huku nikifahamu kuwa nilichofanya ni kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo ya Ushuru wa Mazao ya Misitu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo ya mwaka 2022.
Jina:________________________________saini_____________alama ya dole gumba ____________________________________tarehe_______________________________

Mbele ya:

Jina:___________________________________Saini___________________
tarehe:_________________________________

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi za (Ushuru wa Mazao ya Misitu) kufuatia Azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika mnamo tarehe 11/8/2021 mbele ya:-

LAIN E. KAMENDU,
*Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya,*
*Kilolo.*

ANNA M. MSOLA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya,*
*Kilolo.*

L.S

NAKUBALI,

Dodoma,
2 Machi, 2022

INNOCENT L. BASHUNGWA (MB.),
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi,*